



MASWALI NA MAJIBU KUHUSU MWALIMU COMMERCIAL BANK

1. Je, mikutano ya wanahisa hua inafanyika?

- Ndio Mikutano mikuu ya wanahisa hua inafanyika kila mwaka na taarifa hutolewa kwa wadau wote.

2. Tunawezaje kupata taarifa ya lini mikutano hua inafanyika?

- Taarifa juu ya mikutano huwa inatolewa kwa njia ya magazeti, akaunti za mitandao ya kijamii ya Benki (Instagram/Facebook @mwalmubank), tovuti ya Benki (www.mwalimubank.co.tz) pamoja na ujumbe mfupi kwa njia ya simu kutumwa kwa wanahisa.

3. Je, ni taratibu gani za kufuata pindi Mwanahisa wa Benki ya Mwalimu anataka kuza hisa zake?

- Mwanahisa anaweza kuza hisa zake kwa Wakala yeyote aliyeorodheshwa kwenye soko la hisa (DSE), atatakiwa kuwa na kitambulisho pamoja na cheti cha hisa.

4. Je, naweza kununua hisa za Mwalimu Benki?

- Ndiyo, unaweza kununua hisa muda wowote kupitia kwa wakala yeyote aliyeorodheshwa kwenye soko la hisa (DSE), utatakiwa kuwa na kitambulisho pamoja na cheti cha hisa.

5. Je, mna mpango gani wa kuhakikisha watu ambao hatujapata vyeti vya hisa tunavipata?

- Walimu wote ambao hawajapata vyeti, wanaweza kupata vyeti vyao kupitia kwa;
 - ❖ wakala wa soko la hisa Core Securities
 - ❖ viongozi wa Chama cha Walimu
 - ❖ kupitia kwa afisa wa benki namba 0768025671
- Pia kwa kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia ambayo inatumia mifumo ya kidigitali zaidi, benki ina utaratibu wa kuhifadhi taarifa zote za msingi za wanahisa wake ambapo mwanahisa hata kama hajapokea cheti chake anaweza kuona taarifa zake zote kwenye regista ya bank. Utaratibu huu pia unatumika kwenye makampuni na mashirika mengine makubwa ambapo yametoka kwenye mfumo wa makaratasi na kwenda kidigitali mfano, makampuni ya bima na TRA

6. Toka benki ianzishwe imemfaidisha vipi mwalimu na hisa alizonazo?

- 95% ya wakopaji ni walimu, riba na gharama nafuu, mikopo maalumu kwa wastaafu na waajiriwa wapya.
- Tumeweza pia kuwafikia walimu na kuwapatia huduma kwa urahisi zaidi kwa kuongeza vituo vya kutolea huduma, ambapo tulianza na vituo viwili na sasa tuna jumla ya vituo saba. Benki inakaribia kuanza kutoa gawio katika mpango mkakati wa 2021-25

7. Benki imepata faida gani na mwalimu amefaidikaje?

- Benki imeanza kutengeneza faida kuanzia mwishoni mwa mwaka 2021 pia utoaji wa mikopo umeongezeka ambapo walimu wengi wamenufaika na wanaendelea kunufaika na amana zimeongezeka kutoka kwa wanahisa ambao asilimia kubwa ni walimu.
- Benki imeweza kuboresha mifumo MwalimuCard VISA, MwalimuMobile na Mawakala Zaidi ya 200 nchi nzima.
- Mwalimu amewekeza na kuendelea kupata huduma bora na rahisi.

8. Nani mmiliki hasa wa benki hii kati ya mwalimu na wanahisa wengine?

- Wamiliki wa benki ambao ndio wanahisa ni kama wafuatavyo;
- | | |
|----------------------|-------|
| ❖ Walimu waanzilishi | 35.3% |
| ❖ CWT | 12.9% |
| ❖ NHIF | 16.2% |
| ❖ PSSSF | 16.2% |
| ❖ Umma kwa ujumla | 16.2% |
| ❖ TDCL | 3.2% |

Walimu kwa ujumla, CWT na TDCL ni 51.4%

9. Kwa wale tulionunua hisa wenyewe na pia zingine kununuliwa na CWT na kwa bahati mbaya tukawa hatujapewa vyeti vya hisa, je zitakuwa zimeorodheshwa kwenye cheti kimoja?

- Hapana, hisa zitaorodheshwa kwenye vyeti viwili tofauti kulingana na ununuzi wake.

10. Ni utaratibu gani utakaoniwezesha kulifikia soko la hisa kwa kuuza au kununua hisa za MCB nikiwa huku kijijini?

- Kuna njia mbili za kuweza kuuza au kununua hisa; ya kwanza ni kupitia Aplikesheni ya simu ya Wakala wa soko la hisa (DSE Hisa Kiganjani) na ya pili ni kwa kuandika barua ya kuuza au kununua hisa ukitaja idadi ya hisa, bei ya kuuzia, taarifa za benki ya kufanyia malipo ya hisa hizo pindi zitakapouzwa pamoja na nakala ya kitambulisho cha utaifa. Barua hiyo itatumwa kwa moja ya madalali wa kuuza hisa utakayemchagua kwa ajili ya kukuuzia hisa zako.

11. Pamoja na kuwa hisa zinarithishwa/ kuhamishwa ni utaratibu gani unatumika ili kuhamishia hisa kwa mtu ninayetaka kumpa (hisa zote au kiasi?)

- Mwanahisa anaweza kurithisha au kuhamisha hisa zote au kiasi kwa mtoto au mzazi tu. Atahitajika kuandika barua ya kurithisha au kuhamisha hisa zake akitaja dhumuni au sababu ya kuhamisha, akiambatanisha cheti cha kuzaliwa mtoto na kitambulisho chake kama anahamishia kwa mtoto na kama anahamisha kwa mzazi, mwanahisa ataambatanisha cheti chake cha kuzaliwa pamoja na nakala ya kitambulisho cha mzazi na cha kwake. Barua hiyo itatumwa kwa wakala wa soko la hisa ambaye atajaza fomu maalumu na kufanya uhamisho huo.

Kwa mawasiliano zaidi tupigie huduma kwa wateja namba: 0800750033.

Kurasa za kijamii: facebook/Instagram/twitter @mwalimubank , LinkedIn @Mwalimu Commercial Bank

Tovuti: www.mwalimubank.co.tz

Barua pepe: info@mwalimu.co.tz